

KILIMO CHA BINZARI

By Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika



Utangulizi Jina la kitalaam ni *Curcuma domestica* na kwa kiingereza ni turmeric. Zao hili asili yake ni Mashariki ya Mbali, na linalimwa zaidi katika mkoa wa Tanga, Kagera, Kilimanjaro, Morogoro na Zanzibar.

Matumizi

Binzari hutumika kwa mapishi ya nyama, samaki na mapishi mengine kwa kuweka rangi yake ya njano. Hutumika zaidi na nchi za mashariki kama India; nchi za Ulaya hutumia kidogo sana.

Uzalishaji

Hali ya hewa Humea vizuri maeneo yenye kiasi cha joto la nyuzi 24-26 za sentigredi na huzalishwa maeneo ya mwambao.

Udongo

Udongo wenye rutuba na unaopitisha maji na usio na mawe au changarawe.

Mahitaji ya mvua

Mahitaji ya mvua ni milimita 1200-2000 kwa mwaka. Epuka kusimama kwa maji shambani. Umwagiliaji unaweza kufanywa endapo maji hayatoshelezi. Binzari inafanya vizuri ikipandwa sehemu ya uwazi. Ingawa pia inaweza kuchanganywa na mazao mengine kama minazi.

Uchaguzi wa mbegu.

Mbegu zinazotumika hapa nchini ni za kienyeji bado. Tunguu kubwa zenye ukubwa wa sm 2.5 hadi sm 3 hutumika kama mbegu. Kiasi cha tani 1.7 za vipando huhitajika kwa hekta. Tunguu za kupandwa zisihifadhiwe kwa zaidi ya mwezi mmoja kabla ya kupanda.

Nafasi ya upandaji

Nafasi ya kupanda ni sm 30-45 kati ya mmea na mmea.

Mahitaji ya mbolea

Matumizi ya mbolea hapa Tanzania si makubwa katika kilimo cha viungo. Tafiti zimeonesha kuwa binzari hazioneshi kufanya vizuri kwenye mbolea za viwandani. Mbolea za samadi zinaweza kutumika.

Uvunaji

Uvunaji hufanywa kwa kutumia majembe au uma. Binzari huvunwa wakati majani yamegeuka angina kuwa njano au kahawia. Binzari isiyo na kambamba huvunwa kipindi cha miezi sita toka kupandwa na miezi 18 hadi 21 kwa binzari iliyokomaa kutegemeana na mahitaji ya soko. Mavuno ya tani 7 hupatikana endapo binzari ikipandwa peke yake. Mavuno hupungua kiasi binzari ikipandwa mchanganyiko na mazao mengine kwa mfano mavuno ya tani 4.8 kwa hekta yatapatikana binzari ikipandwa na minazi.

Utayarishaji

Kabla ya kuhifadhiwa binzari huchemshwa, huanikwa juani kisha hutwangwa/husagwa.

Mashambulizi ya wadudu na magonjwa

Tatizo kubwa ni ugonjwa wa ukungu unaosababishwa na vimelea vinavyoitwa *Colletotrichum* sp. na *Glomerellacingulata*. Dalili ni madoa ya kahawia kwenye majani ambayo husambaa na kisha jani hukauka. Magonjwa haya yanaweza kudhibitiwa kwa kupiga dawa za ukungu kama Dithane M-45 kila baada ya wiki mbili.

Masoko.

Soko la binzari linapatikana ndani na nje ya nchi. Bei ya ndani ni inaanzia Sh 500-na kuendelea. Zao hili huuzwa katika nchi za Uganda, Kenya, Uingereza, Ujerumani, Mashariki ya Kati, n.k.

Ushauri

Wakulima wanashauriwa kukausha binzari kwa uangalifu ili kutoharibu ubora wake.

Imepakuliwa :- 26/08/2024

Inapatikana:- https://www.kilimo.go.tz/uploads/Kilimo_cha_Binzari.pdf

:- Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika, S.L.P. 9192, DAR ES SALAAM.

Simu: 022 2864899 Fax : 022 2864899/2862077 E-mail: cps@kilimo.go.tz